
raisingchildren.net.au
the australian parenting website

# Huduma ya kwanza ya kuchomwa na uvimbe wa kuchomwa


ULEZI KWA KUTUMIA PICHA

Inafaa kwa **0-18** miaka


## Kuchomwa na uvimbe wa kuchomwa: jambo la kufanya



**Kuchomwa** ni jeraha katika ngozi ambalo linafanyika kutokana na kugusa kitu moto. **Uvimbe wa Kuchomwa** ni kuchomwa kutokana na viowevu moto.




Iwapo mtoto wako atachomeka au kupata uvimbe kutokana na kuchomwa, kwanza hakikisha eneo hilo ni salama na hakuna hatari kwa mtoto wako au kwako. Mpeleke mtoto wako katika sehemu salama iwapo inawezekana.




Mtoe mavazi yoyote, saa na mapambo karibu na mahali alipochomwa mara moja, iwapo hayajashikilia katika mahali alipochomwa. Yaache malengelenge usiyaguse.


## Huduma ya kwanza ya uvimbe wa kuchomwa na kuchomwa




Tibu kidonda cha kuchomwa na **maji baridi yanayotiririka** kwa dakika ishirini. Iwapo mtoto wako anababaika au anahisi baridi sana, unaweza kupoza mahali alipochomeka kwa dakika kadhaa kila wakati katika saa tatu zinazofuata.



**Poza palipochomeka, sio mtoto**. Iwapo sehemu iliyochomeka ni kubwa, wacha kupoza baada ya dakika 20. Mweke mtoto wako na joto kwa sababu kupungua kwa joto la mwili kunaweza kufanyika haraka kwa watoto.



Funika mahali alipochomeka na kifunga kidonda ambacho ni legevu, ambacho hakishikamani kama vile karatasi ya kufungia vyakula au mfuko wa kuhifadhia unaofungwa kwa zipu. Inua viungo vilivyochomeka ili kupunguza uvimbe na uchungu.


## Huduma ya kimatibabu kwa ajili ya kuchomeka na uvimbe wa kuchomeka




**Usipake** barafu, maji yaliyotiwa barafu, losheni, kutia unyevunyevu, mafuta, dawa ya kupaka, siagi au unga, kirimu au poda katika sehemu iliyochomeka. Hili litafanya jeraha kuwa mbaya zaidi.




**Ita ambulensi** iwapo mtoto wako amechomeka usoni, katika njia ya hewa, mikono au sehemu za siri, au iwapo sehemu aliyochomeka ni kubwa kuliko mkono wa mtoto wako




**Enda ukamtembelee daktari au hospitali** iwapo sehemu alipochomeka inatoshana na kipande cha senti 20 au kubwa, au iwapo imeingia ndani, ni mbichi, mbaya sana au ina malengelenge. Pia enda iwapo uchungu unaendelea au ni mwingi sana, au hauna uhakika kuhusu ukali wa jeraha la kuchomeka.

Burns and scalds first aid (Swahili) © Raising Children Network